

# UNO yamchachafya Mwafrika vikali Mreno

26/7/63

UNO, New York, Alhamisi.

AZIMIO kali linalotazamiwa kulazimisha Serikali ya Ureno itoe uhuru kwa makoloni yake ya Afrika katika muda wa miezi miwili au mitatu, na huenda ikapigwa marufuku asipate kago ya silaha, linatengeneza leo (Alhamisi) katika UNO.

Nchi 12 za Kiafrika na Kiafrika katika UNO ndizo zinazotengeneza azimio hilo; na Mawaziri wanne wa nchi za Kiafrika wanaohudhuria majadiliano katika Halmashauri Kuu ya UNO inayosimamia amani ulimwenguni wanafahamishwa mawazo yanayotolewa katika kazi ya kutengeneza azimio hilo.

Inatazamiwa kuwa nchi za Ghana na Morocco, ambazo ni wanachama wa Halmashuri hiyo, ya amani watafsisha azimio hilo wakati wa majadiliano ya Makoloni ya Kireno.

Wachunguzi wa mambo katika UNO wanadokeza kuwa azimio hilo linatarajia kudai Ureno kuendesha udhalimu katika makoloni yake ya Afrika. Itambue haki ya wanachini kujitawala katika makoloni hayo, iachilie huru wafungwa wa siasa na kishapo ifanye mazungumzo na vionzozi wa vyama vya siasa juu ya kubadilisha ili hatimave uhuru kamili unatikane kati ka makoloni hayo.

Wanadokeza pia kuwa azimio hilo litatoa adhabu mara moja na Mreno ikiwa hata timiza masharti yake kwa muda huo aliopewa wa miezi miwili au mita tu.